

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO MIFUGO NA UVUVI**



TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZA MUDA WA KUTUMA MAOMBI YA
KUJIUNGA NA VYUO VYA KILIMO KWA MWAKA WA
MASOMO 2017/2018**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi (KILIMO) Mhandisi, Mathew Mtigumwe, anawatangazia Watanzania wote kuwa muda wa kutuma maombi ya kujiunga na Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo katika kozi ya Stashahada na Astashahada umeongezwa hadi tarehe **8/8/2017**.

Kuongezwa kwa muda, kutawasaidia Wanafunzi waliochelewa kutuma maombi hapo kabla na sasa wanatakiwa, kutuma maombi kabla ya tarehe tajwa;

Kupitia tangazo hili Wahitimu wa kidato cha sita na wengine wenye sifa za kuomba nafasi hizo, wanatakiwa kutuma maombi yao, haraka iwezekanavyo.

Fomu ya maombi na orodha ya Vyuo vya Kilimo inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi; ambayo ni (www.kilimo.go.tz) au kupitia link hii: - [www.kilimo.go.tz/index.php/en /highlights/view/application-for-admission-into-diplo...](http://www.kilimo.go.tz/index.php/en/highlights/view/application-for-admission-into-diplo...)

Imetolewa na:-

Kitengo cha Mawasiliano Serikali

Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi (KILIMO)